HelpAge International
age helps

# Sheria za mirathi

## Kitini cha Wazee washauri vijijini



BMZ | Federal Ministry for Economic Cooperation and Development

HelpAge Deutschland
Alter ist Zukunft

## UTANGULIZI:

Kitini hiki cha Wazee washauri kimetengenezwa kama sehemu ya mradi wa miaka mitatu wa *''Kulinda na kuwaenzi wanawake wazee na kuwawezesha kijamii na kiutamaduni nchini Tanzania''*. Mradi huu unalenga kuboresha haki za Wazee (hasa Wazee wanawake) kwa kuwawezesha kupitia shughuli mbali mbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa ushauri, kusikiliza malalamiko, na kutoa ushauri nasaha na maelekezo yenye misingi ya kisheria pale inapobidi.

Mradi huu utatekelezwa na shirika la Magu Poverty Eradication Centre (MAPERECE) katika kata nne za Wilaya ya Magu na Kwimba; na Shirika la Saidia Wazee Karagwe (SAWAKA) kwenye kata nne za Wilaya ya Karagwe na Kyerwa. Pia mradi huu unatekeleza mojawapo ya vipaumbele vya Shirika la HelpAge International vya kuwawezesha Wazee wanawake na wanaume kupinga ubaguzi kiumri na kudai haki zao.

Kitini hiki kimetengenezwa ili kitumiwe na watu wenye umri mkubwa na kimeandikwa kwa lugha rahisi ili kuwezesha kuwepo kwa mijadala kati ya Wazee washauri waliopata mafunzo na Wazee watakaohitaji msaada wa kisheria. Maelezo yaliyomo katika kitini hiki yameandikwa kutoka katika Sheria za Mirathi kwa vile sehemu kubwa ya sheria hizi zinahusu masuala ambayo ni ya msingi kwa watu wa aina zote.

Watumiaji wa kitini hiki hasa wanatarajiwa kuwa ni Wazee washauri waliopata mafunzo pamoja na Wazee wengine kwa ujumla. Juhudi za makusudi zimefanyika kuhakikisha kuwa maandishi haya na lugha iliyotumika ni rafiki na imezingatia umri, jinsi, maoni, imani na viwango vya elimu na kwa watu wanaoishi vijijini. Lengo kuu la kitini hiki ni kuwapatia Wazee taarifa rahisi na sahihi za kuwawezesha kutambua masuala yanayoweza kusuluhishwa kwa amani  kwa kutumia mbinu za kienyeji na yale yanayohitaji msaada wa kitaalamu wa kisheria. Kwa hali yoyote ile kitini hiki hakilengi kuwafanya Wazee washauri kudai kuwa wao ni wanasheria ama mawakili, na kwa vyovyote vile hakikutengenezwa kuchukua nafasi ya shughuli za wanasheria ama mawakili waliosomea taaluma hiyo. Kitini kinalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa rahisi na sahihi ili watu wafanye maamuzi ya busara juu ya hatua za kuchukua, na kuepuka migogoro ya muda mrefu na isiyo ya lazima wakati mawazo yaliyo kwenye kitini hiki yangeweza kutoa mwongozo. Tunaamini kuwa taarifa zilizo kwenye kitini hiki zitakuwa na manufaa kwa Wazee na wanajamii wengine wanaohitaji taarifa kuhusu sheria za Mirathi.

## KUHUSU SISI

HelpAge International ni mtandao wa kimataifa wenye njozi ya kuwa na dunia ambamo Wazee wataishi maisha yenye hadhi, afya na nguvu. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa wazee katika nchi ya Tanzania wanapata fursa sawa ya kutumia rasilimali na huduma kama ilivyobainishwa kwenye sera mbali mbali na mifumo ya sheria kwa kuingiza masuala ya Wazee katika mipango ya maendeleo ya nchi hii, na kuondoa umaskini unaowaathiri Wazee na wategemezi wao.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo;

HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street
Regent Estate, Mikocheni
P. O. Box 9846
Dar es Salaam
Tanzania
Email: haitz@helpagetz.org

Magu Poverty Eradication Centre
P. O. Box 333
Magu
Tanzania
Email: maperece@hotmail.com

Saidia Wazee Karagwe
P.O.Box 21
Karagwe
Tanzania
Email: kasawatakaragwe@yahoo.com

## SHUKRANI

Utengenezwaji wa kitini hiki umewezeshwa kupitia msaada wa Wizara ya Ushirika wa Uchumi na Maendeleo ya Shirikisho la Ujerumani, HelpAge Germany na HelpAge International.

## YALIYOMO

1.0 Maana ya mirathi .......... 4

1.1 Sheria ya mirathi ya kimila .......... 4

1.2 Sheria ya mirathi ya kiislamu .......... 6

1.3 Sheria ya mirathi ya kiserikali .......... 7

2.0 Sheria ya mirathi na jinsia .......... 7

3.0 Wosia .......... 8

3.1 Maana ya wosia .......... 8

3.2 Taratibu za kutoa wosia .......... 8

3.3 Aina za wosia .......... 8

3.4 Mambo ya kuzingatia katika kutoa/kuandika wosia .......... 9

3.5 Mahali pa kutunza wosia .......... 9

3.6 Umuhimu wa kuandika wosia .......... 9

3.7 Mifano ya wosia .......... 10

4.0 Taratibu za kufungua mirathi .......... 13

4.1 Wosia ukiwepo .......... 13

4.2 Kama hakuna wosia .......... 13

4.3 Maombi ya usimamizi wa mirathi .......... 14

4.4 Wajibu wa msimamizi wa mirathi .......... 14

## MAANA YA MIRATHI

Mirathi ni utaratibu wa kugawa mali alizoacha marehemu baada ya kifo chake na maelekezo ya jinsi ya kuzigawanya mali hizo au jinsi mali zitavyogawiwa kwa warithi halali. Na utaratibu huu lazima uthibitishwe mahakamani.

Sheria za mirathi zinazotumika Tanzania zimegawanyika katika sehemu tatu:

1. Sheria za mirathi za kimila
2. Sheria za mirathi ya kiislam
3. Sheria za mirathi ya kiserikali

## SHERIA YA MIRATHI YA KIMILA

Sheria hizi zinatokana na mila na desturi za jamii mbali mbali hapa Tanzania. Hali ya kuwepo kwa mila na desturi katika makundi tofauti kulipelekea serikali kuamua kuweka sheria moja ambayo sasa inaitwa sheria za mirathi ya kimila.

Sheria hizi zimepokea nguvu ya kisheria kama sheria nyingine, mradi hazipingani na haki za binadamu.

Sheria za mirathi ya kimila zimegawanyika katika mikondo miwili:-

Urithi unaofuata mkondo wa baba (Patrillineal).

Urithi unaofuata mkondo wa mama (Matrilineal).

Kwa sehemu kubwa sheria za mirathi ya kimila zinafuata mila na desturi za urithi kwa mkondo wa baba.

### Matumizi ya sheria za kimila

Sheria hizi hutumiwa na Watanzania wote wazawa, wasio na asili ya kiasia, kizungu au kisomali.

Endapo itathibitika kuwa mzawa huyu aliacha kabisa mila na desturi za kabila lake wakati wa uhai wake, sheria ya kiislamu itatumika kugawa mirathi yake iwapo marehemu alikuwa muislamu au sheria ya Kiserikali itatumika kugawa mirathi ya marehemu kama si muislamu.

### Ugawaji wa mali katika sheria ya kimila

Ingawa kanuni zinasema kama marehemu ameacha watoto hao ndio watakuwa warithi wa mali ya marehemu, lakini hapa urithi umegawanywa katika madaraja matatu yafuatayo:

### 1 Daraja la kwanza:

Daraja hili humhusu mtoto wa kiume wa kwanza katika nyumba ya mke wa kwanza wa ndoa. Huyu hurithi sehemu kubwa kuliko wote.

### 2. Daraja la pili

Daraja hili huwajumuisha watoto wote wa kiume waliosalia ambao hurithi sehemu kubwa kiasi ya mali.

### 3. Daraja la tatu

Daraja hili huwajumuisha watoto wote wa kike bila kujali umri wao au nafasi yao ya kuzaliwa. Hawa hurithi sehemu ndogo kuliko wote.

Katika kanuni hizo imebainishwa bayana kwamba watoto wa kike hawaruhusiwi kurithi ardhi ya ukoo ila wanaruhusiwa kuitumia mpaka watakapoolewa au kufa, na hawana mamlaka ya kuiuza.

Watoto waliozaliwa nje ya ndoa hawaruhusiwi kurithi mpaka pale itakapothibitika ya kuwa wamehalalishwa kwa kufuata desturi au taratibu zinazojulikana na kutambulika katika jamii hiyo.

### Mjane

Chini ya sheria hii mjane hakuwekewa fungu lake katika urithi. Badala yake anatakiwa kutunzwa na watoto wake jinsi ambavyo yeye aliwatunza.

Hata hivyo jukumu hili la warithi kumtunza mjane haliwawajibishi watoto endapo hawatamtunza mjane.

Mjane mgumba, Sheria ya Hali ya Watu inasema mali ya marehemu itagawanywa nusu na mjane atapewa 1/20 ya nusu ya mali ya marehemu. Pia ana haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa mpaka atakapoolewa na mwanaume mwingine au kufariki.

Vitu pekee ambavyo mjane anaweza kurithi ni vile vidogo vidogo kwa mfano vyombo vya nyumbani.

Kama ilivyo kwa watoto wa kike, mjane harithi ardhi ya ukoo ila huitumia bila kuiuza wakati wa uhai wake.

*Kwa ujumla baadhi ya kanuni zilizomo katika sheria ya urithi kimila zinakiuka haki za binadamu (usawa wa binadamu) na zinawanyanyasa wanawake.*

### Mahali pa kufungulia mirathi za kimila :

Kesi za mirathi ya marehemu kwa sheria za kimila lazima zifunguliwe katika Mahakama ya Mwanzo.

# 2. SHERIA YA MIRATHI YA KIISLAMU

## Sheria ya mirathi ya kiislamu

Sheria hii ya mirathi huwahusu Watanzania wote ambao itadhihirika kuwa wameacha mila na desturi zao na uislamu huwaongoza katika pengele zote za maisha yao; pamoja na watu wengine ambao siyo wazawa lakini ni waislamu.

## Matumizi ya sheria ya mirathi ya kiislamu

Ugawaji wa mali chini ya sheria ya kiislamu huwa rahisi kwa vile viwango tayari vimewekwa katika kitabu cha Korani.
Chini ya utaratibu huo:

- Kama kuna watoto mjane/wajane hurithi moja ya nane (1/8) ya mali.
- Kama hakuna watoto mjane/wajane hurithi robo (1/4) ya mali.
- Mali iliyobaki hugawanywa mafungu matatu kama ifuatavyo:
  - Wale wa kiume hupata mafungu mawili (2/3).
  - Wale wa kike hupata fungu moja (1/3).

Mgane (mjane mwanaume) hupewa ¼ ya mali ya marehemu mke wake kama kuna watoto, au ½ kama hakuna watoto.

Wazazi wa marehemu hupewa 1/6 ya salio baada ya kuondoa fungu la mjane/wajane.

Katika dini ya kiislamu marehemu huruhusiwa kuacha wosia wa theluthi moja tu (1/3) ya mali yake kwa amtakaye. Theluthi mbili ya mali lazima irithiwe na warithi wake ambao ni pamoja na wategemezi wote wa marehemu.

Mtu ambaye sio muislamu hawezi kurithi mali ya muislamu – hata kama ni mke/mume.

Mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa kwa sheria ya Kiisalamu hawezi kurithi mali ya marehemu ambaye alikuwa muislamu.

# 3. SHERIA YA MIRATHI YA KISERIKALI

## Matumizi ya sheria ya mirathi ya kiserikali

Sheria hii hutumiwa na Watanzania wote walioacha mila na desturi zao na ambao si waislamu na watu wengine ambao si wazawa (yaani wageni kutoka nchi nyingine).

## Matumizi ya sheria ya mirathi ya kiserikali

Mgawanyo wa mali katika sheria ya kiserikali huwa kama ifuatavyo:

- Kama kuna watoto, mjane/mgane hurithi moja ya tatu (1/3) ya mali.
- 2/3 ya mali hugawiwa sawa kwa watoto wote wa kike na wa kiume.
- Kama hakuna watoto mjane hurithi 1/2 ya mali.
- 1/2 nyingine ya mali huchukuliwa na wazazi au ndugu wa marehemu wa karibu iwapo wazazi hawapo.

Kwa mtazamo wa haraka watu wengi wangependa itumike sheria ya kiserikali ili mali zao ziendelee kusaidia familia zao. Hata hivyo ni vigumu kuthibitisha kuwa mtu aliacha mila zao na hasa wale wanaoishi vijijini na waliooana kwa ndoa za kimila.

Ikumbukwe kuwa kama marehemu aliacha wosia mali zake zitagawanywa kwa kuzingatia maelezo ya wosia.

# SHERIA YA MIRATHI NA JINSIA

Mpaka hatua hii tayari imejitokeza wazi wazi kuwa baadhi ya sheria za mirathi zimekuwa zikiwakandamiza wanawake na watoto hasa watoto wa kike na hivyo kukiuka haki za binadamu.

Katika maeneo mengine wanawake Wazee wamekuwa wakiuawa kwa visingizio kuwa ni wachawi wakati kiini halisi cha mauaji ni ugomvi wa mali.

Ili kuhakikisha kuwa wajane na watoto hawadhulumiwi haki zao ni muhimu jamii ikaelimishwa umuhimu wa kuandika wosia kisheria.

Hili litapunguza dhuluma wanayotendewa wajane na watoto wao pamoja na utata unaojitokeza wakati wa kuamua ni sheria ipi itumike wakati wa kuamua mirathi ya marehemu.

# WOSIA

## MAANA YA WOSIA

Wosia ni kauli, tamko au maandishi anayotoa mtu wakati wa uhai wake kwa hiari yake, na kuonyesha ni jinsi gani angependa mali yake igawanywe kwa warithi wake baada ya kufa kwake.

Kwa hali hii wosia huepusha migongano ndani ya familia na jamii juu ya ugawaji wa mali za marehemu.

### Lazima mtoa wosia awe na umri wa miaka 18 au zaidi

- Lazima mtoa wosia awe na akili timamu. Mgonjwa aliye katika hali ya kupoteza fahamu hawezi kutoa wosia.
- Wosia unatakiwa utolewe mbele ya mashahidi wawili au wanne kutegemeana na aina ya wosia. Inatakiwa mashahidi wote washuhudie kwa wakati mmoja.
- Ni muhimu mke/wake wa marehemu kuwepo wakati wa kutoa wosia.
- Warithi hawawezi kuwa mashahidi.
- Wanawake pia wanaweza kuandika wosia.
- Wosia hauhusu mali pekee, bali hata maelekezo ya jinsi ya kutumia mali zinazoachwa na marehemu.

## AINA ZA WOSIA

Kuna aina mbili za wosia:
1. Wosia wa maneno
2. Wosia wa maandishi

### Wosia wa maneno

Wosia huu hutolewa na mtoa wosia mwenyewe kwa kutamka mambo ambayo anataka yafanyike baada ya yeye kufa. Wosia huu huwa na mashahidi wanne, ambao wawili hutoka katika ukoo na wawili huwa marafiki zake.

Ikiwa mtoa wosia atataka kufuta wosia wake, atawaita mashahidi wake wote wanne na kufuta wosia huo kwa kutoa wosia mwingine.

### Wosia wa maandishi

Kwa mtu anayejua kusoma na kuandika anatakiwa atoe wosia wake kwa maandishi kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Wosia uandikwe kwa kalamu isiyofutika au upigwe chapa.
- Wosia uonyeshe anwani ya mwosia, kijiji au kitongoji/mtaa anapoishi.
- Tarehe ya kuandika wosia ni lazima iandikwe.
- Pawepo na mashahidi wawili, mmoja aweza kuwa mwana ukoo na mwingine rafiki.
- Inatakiwa mashahidi wote wawili washuhudie kwa wakati mmoja.
- Warithi hawapashwi kuwa mashahidi.
- Ni muhimu kwa mwosia kutaja jina na anwani ya atakayekuwa msimamizi wa mirathi yake
- Ni muhimu mwosia kuandika jina lake na kuweka sahihi yake mbele ya mashahidi wote wawili.
- Pia mashahidi wote wawili wanatakiwa kuandika majina yao na kuweka sahihi zao wakiwa pamoja mbele ya mwosia.

## MAMBO MUHIMU KATIKA KUTOA/KUANDIKA WOSIA

Kisheria mwosia hawezi kumnyima kabisa urithi mrithi halali (mfano mtoto) labda itakapothibitika kuwa mambo yafuatayo yalitendeka:

- Mrithi amezini na mke wa mwosia
- Kujaribu kumuua, kumshambulia au kumdhuru vibaya mwosia au mama yake.
- Kuacha kwa makusudi kumtunza/ kumsaidia mwosia wakati wa shida kubwa kama njaa na maradhi.

## MAHALI PA KUTUNZA WOSIA

Kutokana na ukweli kuwa wosia ni siri, unatakiwa kutunzwa sehemu ambayo ni salama na yenye kumhakikishia mwosia mwendelezo wa siri na pia kutokuwepo na uwezekano wa wosia huo kubadilishwa au kuongezwa maneno na mtu asiye mwosia. Mifano ya sehemu wosia unapoweza kutunzwa ni benki, kanisani, msikitini, kwa wakili.

## UMUHIMU WA KUANDIKA WOSIA

Pamoja na umuhimu wa kuwepo kwa wosia kama ilivyokwisha elezwa, ni muhimu kusisitiza umuhimu wa kila mtu mzima aliyefanikiwa kuwa na mali, hata kama ni kidogo, kuandika wosia.

Ni muhimu sana jamii ikaondokana na fikra potofu kuwa mtu akiandika wosia anajichulia kufa kwani vifo vipo, vilikuwepo na vitaendelea kuwepo maana binadamu wote tutakufa. Hakuna mtu aliyeishi milele kwa vile hakuandika wosia. Wala hakuna ushahidi kuwa watu wanaoandika wosia wanakufa mapema kuliko wale wasioandika wosia.

Siku hizi watu wanakufa sana kwa ajali, magonjwa n.k. hivyo mtu anayeijali familia yake anapaswa kuiachia wosia unaotambulika ili mali atakazoziacha ziwanufaishe wanafamilia yake.

## MFANO WA KWANZA WA WOSIA

1. Huu ni wosia wangu wa mwisho mimi ………………………… ninayeishi kijiji/mtaa wa……………………..
2. Kwa wosia huu nafuta wosia zote nilizowahi kuandika
3. Namchagua……………………......ambaye anaishi……………kuwa msimamizi wa mirathi yangu. Natumaini ataifanya kazi hii kwa uaminifu
4. Nitakapokufa mwili wangu uzikwe kijijini/mtaani kwetu……………….............................
5. Madeni yangu yote yatakayokuwepo wakati wa kufa kwangu pamoja na gharama za mazishi, yalipwe mara moja.
6. Mali zangu ni shamba ekari 1 lililopo Mtakuja, nyumba 1 iliyo hapa mjini/kijijini, baiskeli 1, ng’ombe 2, mbuzi 6, akiba zangu za benki zilizopo CRDB tawi la …………..… akaunti namba ……………………..............………..............................…………............................... ....

Natamka kuwa mali zangu zote zinazohamishika na zisizohamishika zitamilikiwa na mke/mume wangu aitwaye ……………………..............iwapo atakuwa hai baada ya kufa kwangu.

Iwapo mke wangu huyo atafariki mapema kuliko mimi, mali zangu zitarithiwa na watoto wangu wafuatao katika mafungu yaliyo sawa:

a) ……………………………........…………

b) ……………………………........…….…

c) ……………………………........….......

Imetiwa sahihi hapa kijiji/mtaani ………………………tarehe ……………………..........………

Sahihi ya mwosia……………………….......................................................................................

Shahidi wa kwanza: Jina: ………………………………………………………..........……......

Sahihi:………………………………………………........……….................................................

Anwani: …………………………......................................................…...............................................

Kazi yake: ……….............................................……………..............................................................

Shahidi wa pili: Jina: ……….....................................………….....................................................

Sahihi:…………………….........................…........…………......................…...........................

Anwani: …………………………….............................................................................................

Kazi yake: ……………………………….......................................................................................…

Mbele ya: ....................................................................................................................................

Mshuhudia viapo/sahihi...........................................................................................................

## MFANO WA PILI WA WOSIA

1. Mimi ……………wa kijiji/mtaa wa …………kwa hiari yangu, nikiwa na akili timamu, natamka kuwa huu ndiyo wosia wangu wa mwisho na kwa wosia huu nafuta wosia nyingine nilizowahi kuandika

2. Ninamchagua………………………wa kijiji/mtaa wa …………………. kuwa msimamizi wa mirathi yangu

3. Nitakapokufa mwili wangu uzikwe hapa kijijini/mjini ……...............................................

4. Nitakapokufa napenda mgao wa mali zangu uwe kama ifuatavyo:

5. a) Mke wangu aitwaye…………apewe nyumba yetu iliyo ……………, shamba ekari 2 lililo ……...….........,                    ng'ombe 1 na mbuzi 2

6. b) Mwanangu wa kwanza wa kiume aitwaye ………..apewe nyumba 1 iliyo………, shamba ekari 1 lililo                 ………… na mbuzi 2

7. c) Binti yangu mkubwa aitwaye ………….apewe n'gombe 2, mbuzi 1 na kondoo 1

8. d) Mwanangu wa kiume mdogo aitwaye ……..apewe shamba ekari 1 lililo ……..,mbuzi 2 na shilingi                          500,000/= za ada ya shule kutoka kwenye akiba yangu iliyo benki ya CRDB tawi la ……….........................

9. e) Binti yangu wa mwisho aitwaye ………apewe mbuzi 3, kondoo 1 na shilingi na 800,000/= kutoka kwenye akiba yangu iliyo benki ya CRDB tawi la …………kwa ajili ya ada yake ya shule

Sahihi ya mwosia………………………………….. Tarehe …………………..........................

Shahidi wa kwanza: Jina: …………………………………………………….........…...……

Sahihi:……………………………………….................................................................

Anwani: ……………………….....................................……..........................................

Kazi yake: ………..............................……………...…...................................................

Shahidi wa pili: Jina: ………………….........................................................................

Sahihi:…………………............................……………........................................................

Anwani: …………………………...............................................................................

Kazi yake: ……………………………………...............................…...................................

Mbele ya: ..................................................................................................................

Mshuhudia viapo/sahihi...............................................................................................

# TARATIBU ZA KUFUNGUA MIRATHI

## Wosia ukiwepo

- Mtu anapokufa tu kifo kiandikishwe kwa mkuu wa wilaya katika muda usiozidi siku 30, kuthibitisha kuwa kweli mtu anayehusika alifariki.

- Msimamizi wa mirathi aliyetajwa katika wosia au atayependekezwa na kikao cha ukoo akafungue mirathi mahakama ya Mwanzo akiwa na wosia ulioachwa pamoja na cheti cha kifo na muhtasari wa kikao cha ukoo.

- Mahakama hutoa tangazo la mirathi kwa muda wa siku 90 na kama hakuna pingamizi msimamizi hukabidhiwa barua ya kuhalalisha kugawa urithi na kulipa madeni.

- Msimamizi hugawa mali kwa kufuata wosia.

- Baada ya ugawaji msimamizi anatakiwa kisheria kurudisha nakala ya ugawaji mali mahakamani na mahakama hufunga jalada la mirathi hiyo.

## Kama hakuna wosia

- Kifo kiandikishwe kwa mkuu wa wilaya katika muda usiozidi siku 30, kuthibitisha kuwa kweli mtu anayehusika alifariki.

- Mkutano wa ukoo ufanyike kuchagua msimamizi wa mirathi.

- Msimamizi aende mahakamani kufungua mirathi akiwa na nakala ya uamuzi wa ukoo pamoja na cheti cha kifo.

- Mahakama hutoa tangazo la mirathi kwa muda wa siku 90 na kama hakuna pingamizi msimamizi hukabidhiwa barua ya kuhalalisha kugawa urithi na kulipa madeni.

- Msimamizi hugawa mali kwa kufuata maamuzi ya kikao cha ukoo.

- Baada ya ugawaji msimamizi anatakiwa kisheria kurudisha nakala ya ugawaji mali mahakamani na mahakama hufunga jalada la mirathi hiyo.

## BARUA YA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI

### Barua ya maombi ya usimamizi wa mirathi lazima itaje yafuatayo:

- Familia ya marehemu na ndugu wote waliokuwa wanamtegemea marehemu na sehemu wanakoishi.
- Aina na idadi ya mali za marehemu.
- Juhudi zilizofanyika kuhakikisha kuwa marehemu hakuacha wosia.
- Maelezo kuhusu maskani ya marehemu na maisha aliyoishi.

### Wajibu wa msimamizi wa mirathi

- Msimamizi wa mirathi anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:
- Kuchaguliwa kwake kuwa msimamizi wa mirathi hakumaanishi kuwa amekuwa mmiliki wa mali za marehemu.
- Yeye ni mdhamini tu wa kuhakikisha kuwa mali ya marehemu inagawiwa kwa warithi halali.
- Hapashwi kuchukua mali yoyote ya marehemu kwani yeye si mrithi katika mali hiyo.
- Hatakiwi kutumia gharama kubwa za mazishi wakati akijua kuwa marehemu alikuwa na uwezo mdogo.
- Anatakiwa azitumie gharama ambazo ni za lazima ili zibaki fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi mengine muhimu ya familia.
- Ni kutoitendea haki familia ya marehemu ikiwa msimamizi wa mirathi atatoa chakula na mifugo yote kwa ajili ya chakula wakati wa matanga, na baadaye familia ya marehemu ikateseka kwa kukosa mahitaji muhimu.
- Anatakiwa kuzingatia gharama za aina yoyote zilizotumika wakati wa kumwuuguza na kumzika marehemu.
- Anatakiwa kukusanya mali na madeni yote ya marehemu na kuyalipa.
- Anatakiwa kugawa mali ya marehemu kwa misingi ya haki.

- Baada ya kukamilisha shughuli nzima, anatakiwa kutoa taarifa kuhusu vipengele vifuatavyo :

  – Mali na thamani ya mali alizogawa.

  – Madeni yaliyolipwa.

  – Matumizi mbalimbali.

  – Mchanganuo wa jinsi mali ilivyogawiwa kwa warithi.

HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street, Regent Estate, Mikocheni
P.O. BOX 9846 Dar es Salaam Tanzania
Tel: +255 22 2774796/2700169
Fax: +255 22 2775894

Email: haitz@helpagetz.org
Website: www.helpage.or

Copyright © HelpAge International 2014
Registered charity no. 28810